Simu +255 26 23 22965
Nukushi: +255 -26- 2322965
Barua pepe:katibumkuu@ccm.or.tz

Ofisi ya Makao Makuu
Mtaa wa Kuu
S.L.P 50,
Dodoma.

# TAARIFA KWA UMMA

## SALAMU ZA POLE NA RAMBIRAMBI KUFUATIA KIFO CHA SPIKA WA BUNGE MSTAAFU, JOB NDUGAI

Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimepokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Kongwa, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, kilichotokea leo tarehe 6 Agosti 2025 jijini Dodoma.

Kifo cha Mheshimiwa Ndugai, ambaye pia aliwahi kushika nafasi za uongozi ndani ya CCM, ikiwa ni pamoja na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, ni pigo kubwa kwa Taifa letu. Tumempoteza kiongozi shupavu, mzalendo wa kweli na mtumishi mahiri wa umma ambaye alitoa mchango mkubwa katika kuimarisha taasisi ya Bunge na kuendeleza misingi ya demokrasia nchini.

Kwa niaba ya Chama Cha Mapinduzi, tunatoa pole za dhati kwa familia ya marehemu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson, wananchi wa Kongwa na Watanzania wote kwa ujumla kwa msiba huu mzito.

CCM itamkumbuka Mheshimiwa Ndugai kwa uadilifu wake, uthubutu, na moyo wa kizalendo aliouonesha katika kipindi chote cha utumishi wake kwa CCM na Taifa letu kwa ujumla, kwa kusimama imara katika kulinda maslahi ya umma na kuendeleza utawala wa sheria na haki.

Bwana alitoa, Bwana ametwaa; jina la Bwana lihimidiwe.

**KIDUMU CHAMA CHA MAPINDUZI**

Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi
**Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)**
06 Agosti 2025